kumekucha @kumekucha @kumekucha

mwanzo mpya

# KUMEKUCHA

Tovuti: www..kumekucha.co.tz I ISSN 4562.9710 Toleo Na. **0016 JUMATATU 10, 2025** / BEI 1,000 Ksh 100

## Bodi wakala wa vipimo wampongeza Dk. Samia

>SOMA UK. 3

# DK. Biteko awaasa Waislamu kuhifadhi Qur'aan Tukufu

>SOMA UK. 2

**Aipongeza** Al- Hikma kwa kukuza Mashindano ya kuhifadhi Qur'aan**, Mashindano** ya Qur'aan kufanyika Machi 16, **Mashindano** ya Qur'aan Afrika yawa mashindano Makubwa zaidi ya Qur'aan Tukufu Ulimwenguni





## Bado siku 10 tu shida ya maji Tabata, Segerea, Kinyerezi ibaki historia

>SOMA UK. 2



## Kwaheri Sam Nujoma 1929-2025

>SOMA UK. 3



# Wassira aionya Chadema

>SOMA UK. 2

# DK. Biteko awaasa Waislamu kuhifadhi Qur'aan Tukufu

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amewaasa waislamu nchini kuendelea kumcha Mungu na kutenga muda wa kujifunza na kuisoma Qur'aan Tukufu ambayo itawafunza mambo mema yaliyoelekezwa na Mwenyezi Mungu.

Dkt. Biteko amesema hayo jana jijini Dar es salaam wakati akizindua Mashindano Makubwa zaidi ya Qur'aan Tukufu Ulimwenguni 2025.

" Nawaomba msivunjike moyo akitokea mwenye tafsiri tofauti nyie msivunjike moyo wala kukatishwa tamaa bali mfanye mashindano haya yawe kinara na kuutangaza uislamu katika ulimwengu," amesema Dkt. Biteko.

Pia amewahimiza kumuomba Mungu ili Qur'aan iwanyanyue na isiwabwage katika shughuli mbalimbali wanazofanya kama kaulimbiu ya mwaka huu inavyosema " Qur'aan Ikunyanyue, Isikubwage".

Alisema Qur'aan inatoa funzo kwa watu na kuwa waasisi wake waliyaanzisha kwa ngazi ya madrasa lakini baadaye kutokana na umuhimu wake yakavutia wengi zaidi na kuwa mashindano ngazi ya mtaa, kata, wilaya, mkoa hadi kuwa ya Afrika Mashariki, Bara la Afrika na kisha kufikia ngazi ya kuwa mashindano ya Ulimwengu.

" Mashindano haya mbali na kuwa yanachochea usomaji wa Qur'aan Tukufu na hivyo kujenga uelewa wa hofu ya Mwenyezi Mungu lakini pia yanaitangaza Tanzania katika taswira chanya," amebainisha Dkt. Biteko.

Alisema,kuwa Nabii Musa aliwalingania watu wake kwa kutumia muongozo kutoka katika Taurati, Nabii Daudi yeye akatumia Zaburi, Nabii Issa (Yesu) akatumia Injili na Mtume Muhamad swalla llahu alayhi wasallam akatumia Qur'aan tukufu kuwalingania watu wa umma wake.

"Kimsingi vitabu hivi vya muongozo vinamfundisha binadamu tabia njema na kumsihi kuzishikilia na kumuonesha tabia zisizofaa na kumuasa kukaa mbali nazo."

Dkt. Biteko amerejea aya katika Qur'aan tukufu sura ya 35, Surat Faatir, aya ya 28 "..kwa hakika wanaomcha Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wanazuoni".

Amefafanua " Aya hii ina maanisha kuwa wale waliopata ujuzi na mafundisho ya Mwenyezi Mungu ambayo yanapatikana katika Qur'aan tukufu na kuyazingatia yale waliyojifunza ndio wanaofika daraja la uchamungu."

Vilevile, Dkt. Biteko ameipongeza Taasisi ya Al- Hikma kwa jitihada zake za kukuza Mashindano ya kuhifadhi Qur'aan Tukufu ulimwenguni.


Mkurugenzi Mkuu wa Al- Hikma na Mwenyekiti wa Mashindano ya Qur'aan Tukufu Ulimwenguni, Sheikh Nurdin Kishk amesema kuwa mashindano hayo yameendelea kukua kila mwaka kutokana na mapenzi ya kuhifadhi Qur'aan.

Aidha, ameishukuru Serikali kwa ushirikiano wake na kwa kuridhia mashindano hayo kufanyika katika Uwanja wa Taifa Machi 16, 2025 ambapo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

" Mashindano haya yanayofanywa na Al- Hikma Foundation yameweka alama ambayo haitafutika na mataifa mbalimbali yameanza kuyaiga. Pia, Mashindano Makubwa Zaidi ya Qur'aan Tukufu Afrika sasa yatajulikana kama Mashindano Makubwa Zaidi ya Qur'aan Tukufu kwa Mabara yote ya Ulimwengu ," amesema Sheikh Kishk

Akizungumza kwa niaba ya Mufti Mkuu wa Tanzania, Sheikh Ali Ngerukwa alisema kuwa Mufti Mkuu yupo tayari kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwemo ya Ali-Hikma katika kutekeleza shughuli zao.






# Wassira aionya Chadema

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Stephen Wasira amevionya vyama upinzani kuacha kuwatumia vijana kutoka mkoani Mara kama nguvu kazi ya kufanya vurugu katika maeneo mbalimbali.

Wasira ametoa onyo hilo jana alipokuwa akizindua ofisi ya CCM Kata ya Nyakonga wilayani Tarime, Mkoa wa Mara.Alisema CCM ina mipango mizuri kuhakikisha vijana hao wanatumia nguvu zao kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kujikwamua dhidi ya umasikini.

'Nataka niwaambie wananchi wa Tarime CHADEMA wakitaka kufanya fujo mahali popote wanakuja kuchukua vijana Tarime...wanapelekwa kufanya fujo kama majeshi ya kukodi, wakitaka kufanya fujo Mbeya wanakuja, Tarima, wakitaka kufanya fujo sehemu Tarime.

"Tunawaambia vijana wa Tarime wana mvua wana jua na Tarime panalimika, kila kitu kinaota tuwasaidie vijana wa Tarime watumie fursa zilizopo...tunawaambia CHADEMA muache kuja kuchukua vijana Tarime, sisi sio eneo la mapambano, vijana wetu sio wa kukodisha kwenda katika mapambano, nasema kama mzee wa Tarime waache kuja kuchukua vijana wa Tarime.

Wasira aliwataka vijana wasikubali kuchukuliwa na kutumika katika vurugu kwa kuwa wakienda huko hupigwa, kuumizwa na hata kupata ulemavu kisha kurudishwa Tarime wakiwa na hali mbaya.

"Nasema kama mzee wa Tarime, Mzee wa kimila, muache mambo haya mimi najua yanafanyika siku nyingi," alisema.

# Waziri Kikwete akabidhi vijana Hundi ya Tsh. Milioni 700

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Ridhiwani Kikwete amekabidhi hundi ya shilingi Milioni 730 kwa Vikundi 74 vya Vijana, Wanawake na Watu wenye Ulemavu kutoka Halmashauri ya Muheza, jijini Tanga ambayo inatokana na mikopo ya asilimia 10 kupitia mapato ya ndani.

Akizungumza wakati wa kukabidhi hundi hiyo jana,Kikwete,alisema,utaratibu wa kutoa Mkopo kwa makundi hayo umekamilika hivyo kwa sasa kikundi au mtu mmoja anayekidhi vigezo ataweza kunufaika na Mkopo huo.

Ridhiwani amebainisha kuwa, vikundi vilivyonufaika na mkopo huo vimepatiwa elimu ya ujasiriamali na matumizi mazuri ya pesa ili kukua zaidi na kuepuka changamoto zilizokuwepo awali ikiwemo kubadilisha matumizi ya Mkopo huo na kufanyia mambo mengine hivyo kupelekea wakopaji kutorejesha pesa hizo kwa wakati au kushindwa kulipa kabisa.

Alisema Serikali ya Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kuwezesha makundi mbalimbali mikopo yenye riba nafuu ikiwemo mikopo ya asilimia 10.Katika hatua nyingine,Ridhiwani aliwataka wanufaika wa mkopo huo kurejesha pesa hizo kwa wakati ili wengine waweze kukopeshwa.

# TAWA yakabidhi madawati 295 kwa shule za mkoa wa Simiyu

**Na Mwandishi wetu - Simiyu**

SERIKALI kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania - TAWA imekabidhi madawati 295 yenye thamani ya Shillingi Millioni 25.9 Kwa shule za sekondari na msingi Mkoani Simiyu hatua inayolenga kuboresha mazingira ya elimu kwa shule zinazozunguka Pori la Akiba Maswa kama sehemu ya ujirani mwema kati ya TAWA na jamii.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani humo Afisa Habari wa TAWA Beatus Maganja amesema TAWA Kwa kushirikiana na Kampuni ya uwindaji wa kitalii BUSHMAN SAFARI TRACKERS wametoa madawati 295, meza (2) na viti viwili (2) Kwa shule za msingi na sekondari zilizopo wilaya za Itilima na Bariadi ambapo wilaya ya Itilima imepata madawati 190, meza 1 na kiti kimoja (1) na wilaya ya Bariadi imepata madawati 105, meza 1 na Kiti kimoja (1).

Maganja amesema TAWA imekuwa na utaratibu wa kurejesha faida zinazotokana na shughuli za uhifadhi kwa jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi zilizo chini ya usimamizi wa taasisi hiyo, na kwa Mkoa wa simiyu madawati hayo yametokana na mapato yanayotokana na shughuli za uhifadhi zinazofanyika katika Pori la Akiba Maswa.

Aidha amewaomba wananchi wa Mkoa wa Simiyu kuendelea kushirikiana na Serikali katika kulinda rasilimali zilizopo mkoani humo ili kuendelea kufaidi matunda yatokanayo na rasilimali hizo Kwa faida ya kizazi kilichopo na vizazi vijavyo.

Kwa upande wao Kaimu Mwalimu Mkuu wa Shule ya Lung'wa Exavery Lusajo Mwasomola na Mwalimu Stephano Palangyo wameshukuru kwa msaada wa madawati 100 na kukiri kuwa umesaidia kutatua changamoto ya upungufu wa madawati kwa asilimia 100 na kuzidi kuomba msaada zaidi wa kujengewa hosteli, maabara na nyumba za walimu.

# Bado siku 10 tu shida ya maji Tabata, Segerea, Kinyerezi ibaki historia

**Na Juma Kasesa**


ZIMESALIA siku 10 tu kabla ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam(DAWASA)kumaliza tatizo la maji kwa wakazi wa Tabata,Segerea na Kinyerezi.

Wakazi wa maeneo wamekuwa kwenye kadhia ya ukosefu wa maji kwa muda mrefu lakini sasa ni rasmi tatizo linakwenda kumalizika baada ya DAWASA kukamilisha mradi wa upelekaji maji kwa maeneo hayo kwa asilimia 99.

Kaimu Mkurugenzi wa DAWASA,Mkama Bwire amewaeleza wananchi wa maeneo hayo kwamba kuanzia Februari 20 mwaka huu watafungulia rasmi maji ili kuwaondolea kero hiyo ya muda mrefu.

Bwire alisema,serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dk.Samia Suluhu Hassan imedhamiria kuwaondolea kero ya maji Wananchi wake kwa kutoa fedha za ukamilishaji miradi mbalimbali ikiwemo huo wa ambao unakwenda kuwa mwarobaini wa tatizo la maji kwa wakazi wa maeneo hayo.



# Kwaheri Sam Nujoma 1929-2025

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa kwanza wa Namibia huru, Sam Nujoma, amefariki dunia akiwa na miaka 95 katika mji mkuu wa Windhoek, kiongozi wa sasa wa nchi hiyo ametangaza.

Nujoma aliongoza vita vya muda mrefu vya kudai uhuru kutoka kwa Afrika Kusini mwaka 1990 baada ya kusaidia kupatikana kwa vuguvugu la ukombozi la Namibia lililojulikana kama South West Peoples' Organization (Swapo) miaka ya 1960.

Baada ya uhuru, Nujoma alikua rais mwaka 1990 na aliongoza nchi hadi 2005.

Nujoma alikuwa amelazwa hospitalini kwa muda wa wiki tatu zilizopita kutokana na ugonjwa ambao "hakuweza kupona", Rais wa Namibia Nangolo Mbumba alisema katika taarifa yake akitangaza kifo hicho kwa "huzuni na masikitiko makubwa".

Aliongeza: "Baba yetu mwanzilishi aliishi maisha marefu na yenye matokeo ambayo alitumikia kipekee watu wa nchi yake anayoipenda."

Nujoma alistaafu kama mkuu wa nchi mwaka 2005, lakini aliendelea kukiongoza chama hicho kabla ya kung'atuka mwaka 2007 kama rais wa chama tawala cha Swapo baada ya kukiongoza kwa miaka 47.

# Bodi wakala wa vipimo wampongeza Dk. Samia

**Na Veronica Simba**

MKANDARASI wa Jengo la Wakala wa Vipimo(WMA) leo anarajiwa kukabidhi jengo la Ofisi Kuu ya Wakala huyo lililo jijini Dodoma.

Februari 7 mwaka huu ya Bodi ya Wakala wa vipimo ilifanya ziara ya kukagua ujenzi wa jengo hilo na kuridhishwa na kazi iliyofanywa na mkandarasi ambaye aliahidi Februari 10 kukabidhi wahusika.

Mwenyekiti wa Bodi, Prof. Eliza Mwakasangula alisema hatua iliyofikiwa katika ujenzi husika, imewadhihirisha pasipo shaka kuwa litakabidhiwa katika hali ya ukamilifu kama walivyoliona.

"Tumeridhishwa sana na kazi iliyofanywa na Mkandarasi kwa kushirikiana na Mshauri Elekezi. Kinachofanyika sasa ni kukamilisha kazi ndogo ndogo zilizosalia. Kwa hatua iliyofikiwa, hatuna shaka kufikia Febaruari 10 mwaka huu ambayo ndiyo siku ya kukabidhiwa rasmi, Jengo litakuwa limekamilika kwa viwango stahiki," amesema.

Aidha, Prof. Mwakasangula amemshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutenga bajeti ya ujenzi wa Jengo hilo ambalo limegharimu takribani shilingi bilioni 6.2 ambazo ni fedha za ndani.

Pia, amemshukuru Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Selemani Jafo na Menejimenti yake pamoja na kumpongeza Mtendaji Mkuu wa WMA, Alban Kihulla na Menejimenti yake yote kwa usimamizi mzuri wa jengo hilo.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu Kihulla amewaeleza waandishi wa habari kuwa kukamilika kwa jengo hilo kutatatua changamoto mbalimbali za kiofisi.

"Tumeanza na jengo hili lakini matarajio ni kujenga katika maeneo mengine ili mazingira ya kiofisi kwa wateja wanaokuja kupata huduma yawe mazuri lakini na kwa watumishi pia."

Ametaja faida nyingine ya kukamilika kwa jengo hilo kuwa ni kuwezesha vifaa vya kitaalamu kukaa katika mazingira ambayo ni mazuri ili kuendana na usahihi wa kimataifa.

Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya Ukandarasi ya Mohamed Builders inayojenga jengo hilo, Jaffar Mohamed amemhakikishia Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi hiyo kuwa watakabidhi jengo hilo likiwa limekamilika kama ilivyopangwa.

Wafanyakazi wa Wakala wa Vipimo Makao Makuu, ambao kwa sasa wako Dar es Salaam, wanatarajiwa kuhamia Dodoma hivi karibuni baada ya kukamilika kwa Jengo hilo ikiwa ni kutimiza maelekezo ya Serikali yanayozitaka Taasisi na Mashirika yote ya Umma kuhamia Makao Makuu ya nchi, Dodoma.

# Utajiri unaoiponza Congo huu hapa



**Na Mwandishi Wetu**

ENEO la Kivu ni eneo la kimkakati sana na mabepari wote duniani wanalitolea macho kutokana na utajiri wake.Kivu ina madini ya Coltan ambayo yanatumika kutengeneza simu na laptop. 80% ya coltan yote duniani inatoka Congo (unaweza kugoogle kama huamini). Yani kwa kifupi bila Congo hakuna smartphones wala laptop duniani.

Kivu pia kuna madini ya tin yanayotumika kutengenezea solder za kuchomelea vifaa vya kielektroniki kama radio,TV,simu,nk.Kuna madini ya Tungsten yanayotumika kutengenezea silaha.

Na pia kuna Cobalt inayotumika kutengeneza betri mbalimbali zikiwemo za magari. Kama haitoshi Kivu kuna dhahabu nyingi mno.Eneo la Kivu ni eneo lenye dhahabu nyingi zaidi duniani ambayo bado haijachimbwa (The most unexplored gold site globally).

Kagame aliona fursa. Wakati huo Rwanda ilikuwa imetoka kwenye vita na machafuko ya muda mrefu. Akataka rasilimali za jirani. Lakini atazipataje wakati yeye na Mobutu hawaelewani? Akaamua kumuunga mkono mzee Laurent Kabila.

Lakini akaweka masharti. Nikikusaidia kumng'oa Mobutu, eneo la Kivu Kusini,lenye Watutsi wengi (Banyamulenge),litajitenga na Congo na kuwa nchi inayojitegemea.

Alishapiga hesabu za mbali za kuifanya Kivu kuwa sehemu ya Rwanda baada ya kujitenga DRC. Kabila akasema poa tu. Ashapigana miaka 30 msituni bila mafanikio? Sasa kapata "kamserereko" ka kwenda Ikulu akatae? Kagame nyuma yake walikuwepo Ufaransa na Uingereza akasema twende kwa maandishi. Mkataba ukasainiwa mji mdogo wa Lemera, Kivu Kusini. AFDL ikapewa support ya silaha na pesa, ikaamsha dude kupigana na majeshi ya serikali (FARDC).

Wakati Mobutu anajaribu kupambana na AFDL, vikaibuka vikundi vingine vya waasi zaidi ya 40 kupigana na majeshi ya serikali. Vita ikiwa imepamba moto, Rwanda ikajitosa rasmi kupigana na serikali ya Mobutu kwa kisingizio cha kuwatafuta wanamgambo wa Intarahamwe waliokimbilia Congo.

Uganda nayo ikaingiza jeshi kuwatafuta waasi wa LRA. Mobutu kaona "nini cha kufia" akadaka chopa akatokomea zake Moroco. Kesho yake Mei 17, 1997, Laurent Kabila akatangazwa Rais mpya wa Congo. Vita hii ikabatizwa jina vita vya kwanza vya Congo (1996-1997).



# NEMC amkeni, kelele zinatumaliza mtaani

NA MWANDISHI WETU

RAFIKI zangu Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira(NEMC)sijui wako wapi.Inawezekana wako usingizini lakini wacha niwashtue jambo.Hali ni mbaya huku mtaani.Sio sokoni wala barabarani.Kelele mtindo mmoja.

Siku hizi ukitembea katika jiji la Dar es salaam, hali imekuwa si hali ni makelele mtindo mmoja. Hakuna utulivu kabisa.Ukienda masokoni kila mwenye kibanda chake ana spika na rerding inayoita biashara yake non-stop kuanzia asubuhi saa mbili hadi usiku au jioni mida ya kufunga kazi.

Wakati huohuo kuna magari yanapita mabarabarani yanapiga muziki kwa sauti kubwa ajabu eti yanapromote makampuni fulanifulani.Wakati mwingine yanaweka kambi masokoni au sehemu yenye mkusanyiko mkubwa wa watu na kufungulia maspika yake ya muziki. Yaani ni makelele tupu mijini.

Kwa sasa ukiwa jijini Dar es salaam, unafanya mishe zako hakuna utulivu, huwezi kuconcentrate.Ukiacha hilo,utakutana na bodaboda nao wamefunga mziki mzito, wanapiga singeli mtindo mmoja. Miongoni mwa ajali zinatokea kwa wingi jijini Dar es Salaam moja ya sababu ni kelele za barabani.Ni ngumu kusikilizana wala kusikia mlio wa kitu cha hatari. Wingi wa kelele baada miaka michache ijayo utazalisha walemavu wa masikio wengi kisa ngoma zao za masikio zimepoteza uwezo wa kusikia.Hivyo ni vispika hapo sijazungumzia Baa zinazofungulia muziki non stop katika makazi ya watu.

Noise pollution Dar ni kubwa mno imesababisha watu waumwe vichwa, uwezo wa kusikia kupungua, msongo wa mawazo. Ubora wa maisha umeshuka mno na sababu mojawapo ni Makelele mtindo mmoja.Serikali haina budi kufanya yafuatayo.

1.Kuzuia kila mwenye biashara yake masokoni kuwa na kimtambo cha kupiga kelele kuita wateja. Hivi vispeaker vinafanya maisha ya ufanyaji shughuli masokoni kuwa headache.

2.Serikali ipige marufuku kwa bodaboda kufunga speaker kwenye mabodaboda yao, kwanza haya mamiziki wanayofungulia ni hatari kwa usalama barabarani.3. Serikali ithibiti haya matangazo ya magari ambayo huzunguuka mitaani huku wamefungulia muziki kwa staili ya Disco.

4.Miziki kwenye mabaa iangaliwe upya, limiti ya kiwango cha sauti (decibels) kiwekwe ili kupunguzia wananchi adha.Hali ni mbaya sana.NEMC amkeni jamani.Wananchi tunaumia.

**Wingi wa kelele baada miaka michache ijayo utazalisha walemavu wa masikio wengi kisa ngoma zao za masikio zimepoteza uwezo wa kusikia.Hivyo ni vispika hapo sijazungumzia Baa zinazofungulia muziki non stop katika makazi ya watu.**

# Tuendelee kuiamini CCM, kulinda amani yetu

**Na Mwandishi Wetu**

UIMARA na umadhubuti wa Chama cha Mapinduzi(CCM) chini ya Mwenyekiti wa chama hicho Dk.Samia Suluhu Hassan,ndiyo hasa msingi mkuu wa amani, umoja na mshikamano miongoni mwa Watanzania. CCM ndicho chama kilichobeba hatma, matumaini na mustakabali mwema, wa uhakika na salama wa umoja, amani na utulivu wa waTanzania.

Kukubalika na kuaminika kwa sera na mipango mikakati ya maendeleo kumewaunganisha Watanzania, kuwaleta pamoja na kua kitu kimoja.Ama kwa hakika bila CCM madhubuti, nchi itayumba.

Nia na dhamira njema za viongozi waandamizi wa chama na serikali, hasa kiongozi mkuu wa nchi Dr.Samia Suluhu Hassan, vimeendelea kuliunganisha taifa, kuifungua nchi miongoni mwa mataifa ya ulimwengu na kuifanya Tanzania madhubuti zaidi, inayoaminika na kuheshimika ndani na nje ya mipaka ya Tanzania kwa kiwango cha juu sana.

Tunapoelekea uchaguzi mkuu 2025, ni muhimu sana wananchi wote, kufahamu na kuelewa kwamba, ushindi wa kishindo wa CCM, ni ushindi wa wananchi na waTanzania wote, dhidi ya vibaraka wa mabwenyenye ya magharibi, wenye nia ovu binafsi za kutugawanya kwa maslahi yao binafsi.

Kama Taifa inafaa kuungana na tuendelee kuiamini CCM na kuipa nafasi zaidi ya kuongoza, ili hatimae tuendelee kufurahia matunda ya dhamira na nia njema ya Rais Dr.Samia Suluhu Hassan katika kuulinda umoja wetu, na kwa gharama yoyote ile kuitunza amani na utangamano miongoni mwa waTanzania. Mungu Ibariki Tanzania.

CHAMA CHA MAPINDUZI




# Rais Dk. Samia anavyoifungua Ruvuma kwa kiwango cha lami

**NA ABEL MTANDIKA, SONGEA**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan,ameendelea kutimiza Ilani ya CCM kwa kuendelea kukamilisha miradi ya kimkakati hususan mkoa wa Ruvuma ambao sasa unazidi kung'aa baada ya Barabara zake nyingine kuwekewa mkakati wa kujengwa kiwango cha Lami.

Wakala wa Barabara za vijijini na mijini Tanzania (TARURA)wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma, anasema, wametenga zaidi ya Sh.milioni 468 ili kuendelea na mradi wa ujenzi wa Barabara ya Kihamili-Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya Mbinga kwa kiwango cha lami.

Ujenzi wa Barabara hiyo unalenga kuwaondolea Wananchi adha ya usafiri wanapokwenda kupata matibabu kwenye Hospitali hiyo, kurahisisha huduma ya kusafirisha mazao na kukuza kipato cha Mwananchi mmoja mmoja, wilaya ya Mbinga na Taifa kwa ujumla.

Meneja wa TARURA Wilaya ya Mbinga Oscar Mussa amesema, Barabara hiyo inajengwa kwa awamu na ina urefu wa kilometa 3.4 na kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imejengwa kwa kiwango cha lami urefu wa mita 750.

Aidha Mussa, ametaja kazi nyingine zilizotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na kufungua barabara mpya yenye urefu wa kilometa 3.5 kuelekea makazi mapya ya viongozi wa Halmashauri ya wilaya Mbinga.

Anasema, licha ya kurahisisha usafiri kwa wananchi watakaokwenda kupata matibabu katika Hospitali ya Halmashauri,Barabara hiyo itakuwa msaada mkubwa kwa wanafunzi na wafanyakazi wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) kwenda na kurudi chuoni na kuboresha Barabara katika eneo la Kihamili ambalo ni kioo kwa kata ya Kigonsera.

"lengo kubwa la Wakala wa Barabara za vijijini na mijini(TARURA)ni kuwawezesha wananchi wa kata ya Kigonsera na wilaya ya Mbinga kwa ujumla kupata wepesi katika shughuli zao za kila siku hasa kilimo cha mzao ya chakula na biashara"alisema.

Kwa mujibu wa Mussa, kazi zilizofanyika hadi sasa ni kujenga Barabara kwa tuta kwa kiwango cha lami ambapo mkandarasi anaendelea kujenga mitaro ya kupitisha maji eneo lote la mradi na baada ya kazi hiyo ataendelea kuweka alama za barabarani na kufunga taa.

Mkazi wa kijiji cha Kigonsera Benson Chiwinga anasema,ujio wa miradi ya Barabara unawezesha vijana wengi kupata kazi zinazowapatia kipato na kupata ujuzi ambao baada ya miradi hiyo kukamilika wanautumia kuendelea kujiajiri na kuepuka kushiriki kwenye matukio ya kiharifu.

Ameipongeza Serikali kwa kuleta miradi hiyo,lakini ameomba isichoke kuendelea kuleta miradi katika Tarafa ya Kigonsera ili wananchi waweze kunufaika kwani itawasaidia kupata ujuzi na kuboresha maisha na kukuza uchumi wao.

"Tunaipongeza sana Serikali yetu kwa hiki inachofanya kwani ni msaada mkubwa kwetu sisi Wananchi tunaoishi hasa maeneo ya vijijini,sisi tunaridhika na kufurahi kwa kazi nzuri inayofanywa na Serikali kupitia TARURA"anasema Chiwinga.

Haji Mbawala alisema,awali Barabara hiyo ilikuwa mbaya kutokana na kuwa a madimbwi mengi katikati ya barabara hasa wakati wa mvua hali iliyosababisha shughuli zao za kilimo na usafiri na usafirishaji kuwa ngumu.

NA MWANDISHI MAALUMU




DK. SAMIA Suluhu ndiye mgombea Urais wa CCM mwaka huu.Ni yeye baada ya Mkutano Mkuu wa CCM kumpitisha kupeperusha bendera ya chama hicho kwenye uchaguzi Mkuu wa Rais,Wabunge na Mdiwani utakaofanyika Oktoba mwaka huu.

Jahazi la CCM litaongozwa na yeye Dk.Samia kwa kusaidiana na Dk.Emmanuel Nchimbi.Kupitishwa kwa Dk.Samia ni ishara ya kukubalika kwake katika katika kutekeleza ilani ya CCM na kuiongoza vyema serikali yake katika kuwaletea maendeleo Watanzania.Hili halina ubishi.

Nani anasema anaweza kuthubutu kusema wanawake hawawezi? Mimi ninasema wanawake wanaweza, tena wanaweza kile ambacho wanaume wanaweza hata kuzidi.Kupitishwa kwa Dk.Samia ni salaam kubwa kwa watu wenye kuamini katika mfumo dume.

Ndiyo, Wanawake wamejaaliwa uwezo mkubwa katika kutekeleza majukumu mazito kabisa katika jamii. Mtazamo hasi wa jamii juu ya uwezo wa wanawake umewadunisha wanawake kwa karne nyingi na hata kuonekana kuwa hawawezi.

Jamii hususani jamii ya kiafrika,kwa karne nyingi imeaminishwa kuwa wanawake ni wasaidizi tu tena ni wasadizi wa shughuli za nyumbani na kwenye nafasi ndogo ndogo za uongozi. Kama nilivyotanguliza hapo juu hali hiyo imetokana na mtazamo hasi wa jamii juu ya uwezo wa mwanamke katika nyanza za uchumi na uongozi.

Mtazamo huo hasi ungalipo miongoni mwetu hata sasa. Namna nzuri ya kuondoa mtazamo huo hasi na kuachana na fikra hizo mgando, ni kuwatazama viongozi wanawake na namna walivyoweza kufanya makubwa yaliyoigusa jamii na kuiondoa katika kero ikiwemo umaskini wa kipato.

Tanzania tumepiga hatua kubwa katika kuthibitisha kuwa wanawake wanaweza tena wanaweza sawa sawa na hata kuzidi wanaume. Tunao viongozi wengi wanawake ambao wanafanya vizuri katika sekta za uongozi na uchumi.

Makala hii kipekee itaangazia utawala wa Rais wa awamu ya sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, Mwanamama shupavu na namna alivyobadili mtazamo hasi wa jamii juu ya kile jamii ilichokuwa inakiamini kuwa wanawake hawawezi.

Nafasi ya urais sio ya mchezo mchezo, ni nafasi kubwa ambayo kwa hapa nchini Rais ndiye Amiri jeshi Mkuu wa majeshi ya Ulinzi na usalama. Rais ni muhimili wa nchi na ndiye mwenye dhima kubwa ya kuhakikisha nchi inakuwa salama na wananchi si tu wanashiriki katika shughuli za ujenzi wa Taifa, bali shughuli hizo zinakuwa na tija na zinawainua watu hao kiuchumi na kuwaondoa kwenye lindi la umaskini.

Makala hii itaangazia mazuri aliyoyafanya Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kipindi cha miaka minne madarakani ambayo yanathibitisha uwezo mkubwa aliokuwa nao mwanamke katika nyanza za uongozi.

Machi 19 mwaka huu, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan atakuwa akitimiza miaka minne tangu ashike hatamu za kuiongoza Tanzania. Hatamu hiyo ya uongozi aliyoichukua kutokana na kifo cha Rais wa awamu ya tano, John Pombe Magufuli, kilichotokea Machi 17, 2021.

# Kupitishwa kwa Dk. Samia Suluhu kugombea Urais ni uthibitisho wa uwezo wa mwanamke

Samia alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa muda wa miaka mitano ambapo alionesha uwezo mkubwa wa kiongozi.Kutokana na umadhubuti na uthabiti wa utendaji wa Samia, akiwa makamu wa Rais, Rais Magufuli alimpendekeza tena kuwa mgombea mwenza wake kwa nafasi ya Urais kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 na hatimae kuwa makamu wa Rais mpaka pale Rais Magufuli alipofariki dunia.

Samia aliapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano akiwa ni mwanamke wa kwanza kushika wadhfa huo hapa nchini kwetu na katika ukanda huu wa Afrika Mashariki. Rais Samia anaingia kwenye historia ya Tanzania kwa kuwa Makamu wa kwanza wa Rais mwanamke na Rais wa kwanza mwanamke.

Ukweli ni kwamba Rais Samia licha ya kuwa ni mwanamke, ameimudu vyema nafasi hiyo ambayo aliipokea katika kipindi ambacho hakuwa amefanya maandalizi ya kuchukua dhamana hiyo kubwa. Kipindi ambacho Taifa lilikuwa linabubujikwa na machozi na kutawaliwa na hali ya sintofahamu iliyotokana na huzuni ya kuondokewa na Rais aliyekuwa madarakani.

Lakini kwa ushupavu mkubwa Rais Samia aliweza kulituliza Taifa na kuondoa sintofahamu zote ambazo watanzania walikuwa nazo juu ya hatma ya uongozi wa nchi yao.Rais Samia ameonesha uwezo mkubwa wa kiuongozi unaojali misingi ya utu na usawa,uongozi usio na upendeleo wa kikanda wala wa kitabaka. Kubwa zaidi ameweza kulituliza Taifa na kulibakiza kwenye reli ya amani na utulivu ambazo ndizo tunu zetu za Taifa.

Ukweli ni kwamba uongozi wa Rais Samia umetegua kitendawili cha mwanamke kutoka kwenye kuonekana kuwa hawezi na kuidhihirishia jamii kuwa mwanamke anaweza sawasawa na mwanaume.Rais Samia amedhihirisha kuwa mwanamke anaweza kushika nafasi yoyote ya uongozi kwenye jamii na akakata kiu ya wanajamii hao, kiu ya maendeleo na pakawepo na amani na utulivu.

Uongozi wa Rais Samia katika kipindi hiki cha miaka minne umeonesha umahiri mkubwa katika kuwahudumia watanzania na kuwareshea matumaini makubwa katika kutatua kero zilizokuwa zinawakabili. Kero kama vile upatikanaji wa huduma bora za elimu, afya, miundombinu, maji, siasa, na uongozi.

Ni ukweli usiopingika kuwa Rais Samia kwa muda alikokaa madarakani amezigusa nyanza hizo kwa namna ambayo inawatia matumaini watanzania wa hali ya chini na kuona kuwa wamepata mkombozi wa kweli wa masahibu yaliyokuwa yakiwasibu kwa miaka nenda rudi.

Ukweli ni kwamba huduma duni za msingi katika jamii watu wa hali ya chini ni wahanga wakubwa kwa kuwa hawana uwezo wa kugharamia kupata huduma hizo. Unapozungumzia ubovu wa barabara, upatikanaji duni wa maji, ukosefu wa huduma za afya za uhakika, watu wa daraja la chini au kama tulivyozea kuwaita makabwela ndio wahanga namba moja.

Mathalani katika sekta ya elimu, Rais Samia eneo la elimu ameligusa kwa namna ya pekee ambayo anastahili pongezi. Sera ya elimu na marekebisho yaliyofanywa juu ya zuio la mtoto wa kike aliyepata ujauzito kurejea shuleni ni hatua ambayo imelenga kumkomboa mtoto wa kike na jamii kwa ujumla kwani, kumueleimisha mtoto wa kike ni kuielimisha jamii.

Hatua ya Rais Samia, kufanikisha ujenzi wa madarasa 15,000 nchi nzima, shule za msingi na sekondari, ni hatua ambayo imelenga kuinua sekta ya elimu na imemuondolea mzigo fukara wa Tanzania na imethibisha umathubuti wa Rais Samia katika kupamba na ujinga kwa kuhakikisha kuwa Taifa Tanzania linakuwa na watu walioelimika ambao watamudu kupambana na changamoto za nyakati.

Kwa upande wa huduma za afya ni wazi kuwa Rais Samia madarakani, huduma za afya kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali za rufaa zimeboreshwa kwa kiwango cha kutia matumaini.

Sambamba na hilo ujenzi wa vituo vya afya unaoendelea nchi nzima ni mwendelezo wa tija kubwa kwa wananchi wa Tanzania. Kila mmoja wetu ni shahidi juu ya adha wanazozipata Watanzania hususani wa vijijini kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za afya. Idadi ya wanawake waliofia njiani kuelekea kupata huduma za afya wakati wa kujifungua ni kubwa pia.

Hivyo tunaamini kuwa kasi ya uboreshaji wa huduma za afya ambayo Rais Samia ameionesha inakwenda kuwa mkombozi mkubwa kwa afya ya watanzania.

Ukweli ni kwamba uongozi wa Rais Samia unaaondoa shaka ya uwezo wa mwanamke katika nyanja za uongozi, kwani kipimo kikubwa cha umathubuti wa kiongozi ni namna anavyotatua changamoto za watu anao waongoza.Rais Samia ametatua changamoto nyingi ambazo huenda ziliihitaji zaidi ya miaka mitano. Tanzania sasa inafunguliwa katika diplomasia na mahusiano ya kimataifa.

Uongozi wa mwanamama huyu shupavu umerejesha mahusiano mazuri na nchi wahisani na nyingine ambazo manufaa yatokanayo ni kuongeza wawekezaji katika sekta ya uchumi ambapo wananchi tutanufaika kwa kupata ajira na fursa nyingine za kibiashara.

Rais Samia ameziona na kuzithamini tunu zetu za Taifa, Moja ya tunu hizo ni rasilimali ambazo mwenyezi Mungu ametujaalia. Tumeona namna anavyohangaika kunadi vivutio nyetu mahali pote duniani ili kushawishi watalii wengi zaidi kuja nchini.

Fedha za kigeni zitakazotokana na ujio wa watalii hao zinatusaidia sana kuweza kutunisha hazina yetu hivyo kuwa na uwezo wa kugharamia miradi mingi zaidi ya maendeleo.

Yapo mengi mazuri ambayo Rais Samia anayafanya ambayo yanavunja rekodi ya viongozi wengi waliopita licha ya kuwa yeye ni kiongozi mwanamke. Rais Samia kwa jinsi alivyosimama imara katika uongozi wa Taifa hili ni wazi kuwa anathibitisha nguvu ya mwanamke iliyo sawa na hata kuizidi nguvu ya mwanaume.

Watanzania tuna kila sababu ya kujivunia uongozi wa Rais Samia kwani sambamba na hatua za maendeleo za haraka tunazopiga, tunaendelea kufaidi amani, utulivu na umoja wa kitaifa huku kila mtanzania akiwa amejawa na furaha na matumani tele kwa mustakabali wake.

# UJENZI BWAWA LA KIDUNDA KUMALIZA SHIDA YA MAJI DAR ES SALAAM, PWANI







MKURUGENZI wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam(DAWASA)Mkama Bwire,pichani akizungumza na Waandishi wa Habari kuelezea mikakati ya Mamlaka hiyo kumaliza shida ya Maji Jijini Dar es Salaam na mikoa ya Pwani. Moja ya mikakati hiyo ni ujenzi wa Bwawa la Kidunda unaondelea Mkoani,Ngerengere Morogoro.Picha nyingine tofauti ni Waandishi wa Habari,maofisa wa Dawasa,Mamlaka ya Bonde la Wami Ruvu,walipotembelea kujionea ujenzi wa mradi huo lakini pia kuona uzalishaji wa maji Mto Ruvu.
Picha na Mpiga Wetu.








## Miaka 48 ya CCM

# 4R za Dk. Samia zimeponya majeraha

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Chama cha Mapinduzi (CCM) kikisherehea miaka 48 ya kuzaliwa kwake falsafa ya 4R ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan,imeponya majeraha ya wengi.

Ikumbukwe,Rais Samia aliingia madarakani Machi 19, 2021 kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa awamu ya tano,Dkt John Magufuli.Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikampa Dkt Samia ambaye alikuwa Makamu wa Rais,ikampa nafasi ya kuapishwa kuwa kiongozi mkuu wa taifa hili.

Wakati anaingia madarakani,Rais Samia aliwaahidi Watanzania kwamba ingawa walikuwa wanamlilia Dkt Magufuli, lakini uongozi wake ulikuwa na lengo la kuponya majeraha na kuwafuta machozi Watanzania.

Utekelezaji wa kauli yake ulianzia kwenye marekebisho ya sera zinazoongoza vyombo vya habari, ambapo Rais Samia alilegeza baadhi ya masharti yaliyokuwa yanawabana Wanahabari katika utekelezaji wa majukumu yao.

Kila mwenye akili ambazo hazina mashaka anajua kwamba serikali ilikuwa imeweka baadhi ya masharti magumu katika sera na sheria nzima inayosimamia vyombo vya habari, lakini baadhi ya magazeti yalisimamishwa,lakini pia vyombo vingine vinavyotoa huduma ya habari ikiwemo mitandao ya kijamii vilitikiswa.

Lakini Dkt Samia alijua kwamba mojawapo ya njia nzuri ya kupata maoni kwenye utawala wake ni pamoja na kuruhusu uhuru wa vyombo vya habari kwa kuvipa wigo mpana zaidi  wa kufanya kazi zake.Sio hivyo tu, Rais aliamua kuwapa nafasi wanasiasa kufanya mikutano yao na siasa nyingine za kiungwana bila kuzuiwa na mtu, kama siasa hizo zitakuwa hazivunji sheria.

Wote ni mashahidi, na kila mmoja ameona kwamba mikutano ya hadhara ambayo ilikuwa imepigwa marufuku iliruhusiwa tena, lakini kwa mara ya kwanza katika historia ya siasa za upinzani hapa Tanzania, wanachama wa vyama vya upinzani waliruhusiwa kufanya maandamano ili kufikisha ujumbe wao kwa serikali na jumuiya ya kimataifa.

Lakini katika eneo hilo la siasa, Rais  Samia amemua kuvunja makundi kwa kuwaunganisha tena watendaji mbalimbali wakiwemo wale ambao walikuwa wametupwa nje katika awamu ya tano kwasababu mbalimbali na kuwapa nafasi ili kuleta uwiano.

> **Mashirika na taasisi mbalimbali za umma waliongezewa uwezo wa kufanya kazi zaidi, lakini baadhi yake zikapewa uhuru wa kuamua baadhi ya mambo yake na kusaidia taasisi hizo kuongeza tija zaidi.**

Mashirika na taasisi mbalimbali za umma waliongezewa uwezo wa kufanya kazi zaidi, lakini baadhi yake zikapewa uhuru wa kuamua baadhi ya mambo yake na kusaidia taasisi hizo kuongeza tija zaidi.

Kuelekea miaka minne ya uongozi wa Rais Samia, Tanzania imepiga hatua kubwa lakini wale waliokuwa wanasema wanawake hawawezi kubeba dhamana ya madaraka makubwa ukiwemo Urais, nao wamekuwa mstari wa mbele kumpongeza Rais Samia kwa mambo makubwa aliyoifanyia Tanzania katika miaka yake hii minne.

# Nini kinasababisha makundi ya waasi kushamiri Congo?



MJI wa Goma ulio mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo umekuwa tena kitovu cha mzozo wa kikanda uliodumu kwa miongo kadhaa. Mapigano kati ya kundi lenye silaha linalojulikana kwa jina la M23 na jeshi la Congo yamezidi katika eneo hilo.Kwa sasa mji huo uko chini ya kundi hilo la waasi baada ya kuuteka.

Kundi la M23 ni kundi lenye silaha ambalo lilijitenga na jeshi la Kongo miaka kumi iliyopita kwa madai ya kuwalinda Watutsi ambao kwa muda mrefu walikuwa wakilalamikia mateso na ubaguzi. Wataalamu wa Umoja wa Mataifa wanasema kuwa kundi hilo linaungwa mkono na nchi jirani ya Rwanda, ambayo pia inaongozwa na Watutsi, jambo ambalo serikali ya Rwanda imekuwa ikikanusha mara kwa mara.

Rwanda imesema hapo awali kwamba mamlaka nchini DR Congo inashirikiana na baadhi ya waliohusika na mauaji ya kimbari ya mwaka 1994 dhidi ya Watutsi na Wahutu wenye msimamo wa wastani.Mwaka 2012, waasi waliikalia Goma kwa siku 10 kabla ya kuiacha kufuatia shinikizo la kimataifa.

Baada ya hayo, kundi la M23 lilipata pigo baada ya kushindwa vibaya na jeshi la Kongo likisaidiwa na jeshi la kimataifa ambalo lilishuhudia kufurushwa kwao kutoka nchini humo. Wapiganaji wa M23 kisha walikubali kushirikishwa tena katika jeshi kwa ahadi kwamba Watutsi watalindwa.

Lakini, mwaka 2021, kundi hilo lilichukua tena silaha, likisema ahadi zilikuwa hazijatimizwa.M23 tangu wakati huo wamechukua udhibiti wa maeneo mengi zaidi katika eneo la mashariki kuliko hapo awali. Wataalamu wa Umoja wa Mataifa wanasema Rwanda ina hadi wanajeshi 4,000 wanaofanya kazi pamoja na M23 mashariki mwa Kongo DR.

Likiwa kwenye ufuo wa kaskazini mwa Ziwa Kivu kwenye mpaka wa Rwanda, Goma daima imekuwa kitovu muhimu cha kisiasa na kibiashara.Mji huo una watu zaidi ya milioni moja na kuufanya kuwa moja ya miji yenye watu wengi zaidi Kongo. Kutokana na udongo wake wa volkeno, wenye rutuba kihistoria mji huo umekuwa kituo cha biashara chenye shughuli nyingi na nchi jirani ya Rwanda.

Goma ni mojawapo ya miji mikuu ya uchimbaji madini inayosambaza madini yanayohitajika sana kimataifa kama vile dhahabu, bati, kobalti na koltani na ina barabara muhimu za kimkakati za usafiri wa barabarani na angani. Pia ina kambi kubwa ya walinda amani wa Umoja wa Mataifa suala ambalo limevutia biashara nyingi, mashirika ya kimataifa na balozi.

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo inakadiriwa kumiliki asilimia 70 ya madini ya cobalt duniani, madini muhimu katika kuwezesha betri za lithiamu-ion katika simu za mkononi, magari ya umeme na aina nyingi za sigara za kielektroniki.

Huku ulimwengu unapojitolea kupunguza utoaji wa gesi chafuzi kwa kuhama kutoka kwa nishati ya kisukuku, kuna ongezeko la mahitaji ya vyanzo safi vya nishati.

Tishio la vita vipya vya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo linaweza kuvuruga ugavi wa kimataifa, kupanda kwa bei na kusababisha uhaba katika tasnia ya teknolojia na nishati safi.

Rais wa Kongo Félix Tshisekedi mwaka 2023 alisema kuwa “Goma haitatekwa kamwe”. Ahadi zake za kuhakikisha kuwa mji huo hauna waasi zilikuwa juu kwenye orodha yake ya ahadi kwa watu wa Kongo, ikimaanisha kutekwa kwa Goma kungemuathiri kisiasa kiongozi huyo aliyechaguliwa tena.Tayari Goma haiko mikononi mwake tena.

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo imekata uhusiano wote na nchi jirani ya Rwanda, jambo ambalo limesababisha onyo kutoka kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres kwamba mzozo wa sasa unaweza kuhatarisha kuongezeka kwa vita vya kikanda.

Kuongezeka kwa mzozo kunaweza pia kusababisha uhaba wa rasilimali za kibinadamu ambazo tayari zimepungua kutokana na machafuko mengine.

Wakati M23 inasonga mbele katika eneo la mashariki, maelfu katika vijiji vidogo wanayahama makazi yao na kuelekea katika hospitali za karibu huko Goma, jambo ambalo linawalemea.

Shirika la kutetea haki za binadamu la Human Rights Watch limeonya juu ya kuongezeka kwa hatari kwa raia huku jeshi la Kongo likipambana na waasi wa M23. Kundi la misaada ya kibinadamu linashutumu pande zote mbili kwa kutekeleza unyanyasaji mkubwa dhidi ya raia.

CC:BBC Swahili



# Unajua mbwa anazaa mara ngapi kwa mwaka?

MNYAMA huyu huaminika ndiye mwaminifu zaidi kati ya wanyama wote wanaofugwa nyumbaniKuna wale wanaomfuga pia kwa sababu humchukulia kama 'kipenzi' chao (pet).

Je, wajua mbwa ni kitega uchumi kwa baadhi ya wanaomfuga? Mnyama huyu ametajirisha baadhi ya wafugaji wanaomthamini.Mbwa hawa hufugwa na kutunzwa kwa msingi wa malengo matatu, wale wa kunusa (sneaver dogs), wa kulinda/kuhifadhi usalama (guard dogs) na wa kuongoza (guide dogs) maafisa wa usalama.

Mbwa huzaa mara mbili kwa mwaka ambapo hubeba ujauzito kwa kipindi cha siku 63 (miezi 2).Kwa kawaida mbwa mmoja huzaa kati ya vilebu 8 – 12.

**LISHE**

Anachohitaji mbwa ni lishe bora pekee huku magonjwa yanayomwathiri yakiwa finyu kinyume na wanyama wengine."Lishe ni kiungo muhimu kwa mbwa, hulishwa kwa chakula anachokula binadamu japo kuna vyakula vingine vinavyonunuliwa kwenye maduka,".

Vilebu hulishwa mara mbili kwa siku huku walionenepa na kukomaa wakilishwa mara moja kwa siku. Hulishwa kwa nyama, mifupa iliyosagwa, chakula halisi cha mbwa kinachojulikana kama 'Top dog', punje za mchele, samaki aina ya 'omena' ama masalia ya chakula.

"Chakula chake huchanganywa na vitamini mbalimbali (multi-vitamin) ili kuboresha afya yake, manyoya, meno na mifupa iwe dhabiti na yenye nguvu. Vitamini hivo ni: CAL-VITAMAX yenye madini ya Calcium'.

Ikumbukwe usafi wa makazi ya mbwa ni jambo la muhimu kuzingatia kwa minajili ya kufurusha wadudu kama vile viroboto na kupambana na magonjwa yanayotokana na uchafu.

"Makazi ya mbwa yanafaa kusafishwa na kupuliziwa kwa dawa aina ya dudu dust kila siku ili kufurusha viroboto. Kisha mbwa waoshwe kwa dawa aina ya Dudu Krin mara moja kwa wiki," ashauri, tabibu wa mifugo.

Magonjwa

Magonjwa kwa mbwa ni jambo linalofaa kutiliwa maanani wakati wa malezi yake.

Magonjwa kama vile:
Canine Distemper,
Canine Herpatitis,
Lep Tospirosis,
Parvo Virus (ugonjwa wa kuendesha damu), Rabbies (Kichaa) ndio huathiri mbwa.

"Ili kuepuka athari za magonjwa haya hupewa aina tatu ya chanjo kwa mwaka. Kikubwa azaliwapo na kufikisha Wiki 6 hudungwa chanjo ya Parvo Virus, akiwa na umri wa Miezi 3 hudungwa ya DHLP na anapohitimu.

Miezi 4 hudungwa sindano ya chanjo ya Kichaa (Rabbies),

Kumbuka;Mbali na chanjo hiyo, pia hupewa dawa za minyoo (deworming) kila baada ya miezi 2. Dawa za minyoo hupewa kulingana na umri wa mbwa.


Mbwa aliyefikisha umri wa mwezi mmoja na nusu hupewa nusu tembe ya dawa aina ya Plozin, miezi 6 hupewa tembe moja na aliye zaidi ya miezi minane hupewa tembe mbili.

"Kuna haja ya mbwa kuhusishwa kwenye matembezi ili kunyoosha viungo vyao vya mwili pia waweze wapunge hewa mwanana.

**FAIDA KUBWA**

Usalama (security firms) na wanaowahifadhi kwa minajili ya kuimarisha usalama katika makazi yao na wanyama wa kucheza nao (pets).

# Fahamu tahadhari aliyoitoa Nyerere kuhusu mgogoro wa mashariki ya DRC



WAASI wa M23 wanaoungwa mkono na Rwanda sasa wanaudhibiti na kuuendesha mji wa Goma ambao ndio mkubwa na muhimu zaidi katika eneo la mashariki ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (DRC).

Mji wa Goma ndio makao makuu ya kiutawala wa jimbo la Kivu Kaskazini na baada ya Kinshasa na Lubumbashi, Goma ni mji wa tatu kwa ukubwa nchini DRC.Pia ni kitovu cha biashara kubwa ya madini ikiwa ni pamoja na dhahabu, coltan, bati na biashara za madini mengine kutoka migodi tajiri huko Masisi, Walikale na kwingineko katika mkoa huo.

Hivyo, kuanguka kwa Goma ni dhahiri kuwa ni pigo kubwa kwa serikali ya Kinshasa pamoja na washirika wake. Lakini pia hatua muhimu ya kusukuma ajenda ya kundi la M23 pamoja na washirika wake katika mgogoro wao na serikali ya nchi hiyo.

Swali muhimu zaidi ni kuwa wakati vita ikiendelea – japo M23 wametangaza kusitisha mapigano wakati wakiwa njiani kujaribu kuuteka mji mwingine muhimu wa Bukavu uliopo katika jimbo la Kivu Kusini – je,M23 kuiteka Goma pamoja na miji na vijiji vingine katika majimbo ya Kivu Kaskazini na Kusini kunaweza kuleta suluhu ya vita?

Je, kutekwa kwa mji wa Goma mara hii kutaleta mabadiliko yoyote?

Kujibu swali hili ni muhimu kuangalia kiini cha mzozo wenyewe kwani hii ni mara ya pili kwa M23 kuuteka mji wa Goma. Mnamo mwezi wa Novemba, 2012, M23 iliuteka mji huu kwa siku 10, baada ya majeshi ya DRC kuutoroka, lakini baadaye waliondoshwa na kikosi maalumu cha kulinda amani cha kikanda kilichokuwa chini ya mwamvuli wa MONUSCO ambacho kilijumuisha wanajeshi wa Tanzania, Afrika Kusini na Malawi.

Hali inavyoonesha ni kuwa mwaka huu – tofauti na ilivyokuwa mwaka 2012 – M23 hawana mpango wa kuishikilia Goma kwa muda mfupi –kwa kuwa tayari wamesogeza mstari wa mbele wa mapambano kuelekea Bukavu. Japo katika tangazo lao la kusitisha mapigano la Jumatatu usiku wametangaza kuwa hawana nia ya kuuteka mji wa Bukavu.

Lakini katika tangazo hilo hilo, wamelaani kile walichodai ni jeshi la Kongo kutuma ndege za kivita "kuua watu katika maeneo ambayo yamekombolewa." Kwa mujibu wa M23, ndege hizo zinatokea katika kiwanja cha ndege cha Kavumu ambacho kipo karibu na Bukavu.

M23 pia wameendelea kusisitiza pia kuwa SADC inapaswa kuondoa vikosi vyake (kutoka Afrika Kusini, Tanzania na Malawi) wakisema misheni yao DRC haina uhalali tena.

SADC pamoja na jumuiya nyingine za kikanda na kimataifa zikiwemo Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), nchi zenye Uchumi mkubwa zaidi duniani (G7) na UN wamelaani vita vinavyoendelea na kutaka mapigano yasitishwe. Wote wanalaani waasi kuteka maeneo ya nchi yaliyo chini ya serikali halali ya DRC.

Rwanda, imekuwa ikisisitiza kuwa kinachoendelea DRC ni tatizo la ndani ya DRC na linatakiwa lisuluhishwe na serikali ya nchi hiyo ambayo wanadai imeshindwa kufanya hivyo na kuwalazimu M23 kudai haki zao kwa mtutu wa bunduki.

Waasi wa M23 pia wanailaumu serikali ya DRC pia kuyaunga mkono makundi ya waasi yanayoendesha harakati zao nchini Kongo, wakiwemo wapiganaji wa jamii ya Kihutu kutoka Rwanda waliotorokea DRC mwaka 1994 baada mauaji ya kimbari, kuwaangamiza ili kuwalazimisha kurudi Rwanda, shutuhuma ambazo serikali ya DRC inazikanusha.

Madai hayo mawili pia yanaungwa mkono na Rwanda, na ndiyo chimbuko la nchi hiyo kuhusishwa na kulaumiwa kwa kuwaunga mkono na kuwafadhili waasi wa M23 na harakati zao nchini DRC.

Uhusiano wa karibu wa Rwanda na M23 unathibitika pia kwa ukaribu wa baadhi ya wakuu kundi hilo na utawala wa Kigali. Kamanda mkuuwa kijeshi wa M23 Sultani Makenga, alipigana chini ya Paul Kagame wakati huo akiongoza waasi kutwaa madaraka Kigali dhidi ya iliyokuwa serikali ya Rwanda na kukomesha mauaji ya Kimbari mwaka 1994.

Na baada ya hapo, Makenga pamoja na Banyamulenge wengine waliomuunga mkono Kagame walijiunga na makundi mengine ya wanamgambo na kushirikiana na jeshi la Rwanda kumpindua Mobutu Sese Seko na hatimaye kumuwezesha Laurent-Désiré Kabila kuingia madarakani.

Suala la ubaguzi dhidi ya Wakongomani wanaozungumza Kinyarwanda (Wanyamulenge) lipo tangu enzi ya utawala wa Mobutu Sese Seko, DRC ikiitwa Zaïre. Wanyamulenge wanaozungumza Kinyarwanda wanaopatikana zaidi katika maeneo ya Kivu wamekuwa wakisema wamenyanyaswa tangu miaka ya 1960 na wamekuwa wakiambiwa "warudi nyumbani" Rwanda.

Akielezea chanzo cha tatizo la Wanyamulenge katika mkutano ulioandaliwa New York na taasisi ya amani, International Peace Academy mwaka 1996, aliyekuwa Rais wa Tanzania Mwl. Julius Kambarage Nyerere aliilaumu serikali ya Zaïre kwa kusababisha mzozo wa ya kikabila kwa kushindwa kusitisha unyanyasaji.

Katika kujenga hoja yake, Nyerere alitoa mfano wa kabila la Wamasai wa Tanzania na Wamasai wa Kenya na kusema hawawezi kuambiwa warudi Kenya ama Tanzania kwa kuwa nchi yao ya asili iligawanywa katika makoloni mawili ya Waingereza na Wajerumani na baada ya uhuru wamejikuta wapo katika nchi mbili tofauti.



# Nenda 'Chinga One,'Utatusaidia kule

**Na Zaka Zakazi**

MWAKA 2001, Mohamed Hussein Daima 'Chinga One' alirudi nchini kutoka Mauritius alikoenda kucheza soka la kulipwa.Aliondoka kwenda huko akitokea Yanga, na hakuondoka vizuri hivyo kiongozi mmoja akakataa kumruhusu arudi klabuni hapo.

Akaenda kusaini Moro United ya Morogoro, timu iliyokuwa ikimilikiwa na tajiri Merey Ally Saleh, maarufu kwa jina la Merey Balhabou.Taarifa zilipoenea kwamba Yanga wamemtoa Mmachinga, Simba wakamfuata ili wamsaini...akawaambia kwamba wamechelewa, ameshasaini Moro United.

Jamaa wakasema 'huyo Simba mwenzetu,' tuachie sisi hilo. Wakamfuata kumwambia kwamba wanamuomba Mmachinga.
Tajiri akasema yeye hana tatizo, ataongea naye. Akamuita ofisini na kumwambia."Simba wamekuja wanakuhitaji. Hata mimi naona ni vizuri ukaenda maana utatusaidia sana kule."

Yaani mmiliki wa timu ya ligi kuu akamtoa mchezaii wake nyota aende timu nyingine huku akisema 'utatusaidia sana kule.Na alimuahidi kwamba asiwe na wasiwasi kwamba sababu ataendelea kumlipa mshahara wake ule ule waliokubaiiana.

'Simba wanaweza wasikulipe hela yako, nitakulipa mimi mshahara wake,' tajiri akamalizia.Na kweli, Chinga akaenda Simba na akawasaidia hadi wakawa mabingwa.

# Simba, Yanga mawindoni upya Ligi Kuu Bara





**Na Husna Nassoro**

VITA ya kuwania alama tatu muhimu kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara inaendelea tena leo kwa Mabingwa watetezi Yanga,kukaribishwa na Maafande wa JKT Tanzania wakati kesho Simba watakuwa wenyeji wa Tanzania Prisons uwanja wa KMC Kinondoni.

Yanga watashuka uwanja wa Meja Isamuyo kuwavaa JKT wakipania kuvuna pointi tatu ili kuzidi kujikita kileleni kwa msimamo.Ikumbukwe Yanga wanaongoza Ligi hiyo wakiwa na pointi 45 kibindoni wakifuatiwa na Simba yenye alama 44 na kufanya vita ya kuwania ubingwa msimu huu kunoga mapema.

Yanga itaingia katika mchezo huo ikiwa inataka kuendeleza moto wa ushindi ilionao ambapo mechi iliyopita iliichakaza Fountain Gate mabao 6-1.Kwa upande wa Simba wataingia katika mchezo huo wakiwa na hasira ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 na Singida Fountain Gate mchezo uliopita na hivyo hawatataka kufanya makosa tena mbele ya Tanzania Prisons.

Mpaka sasa Simba na Yanga zimeshajikatia kipande chao cha mbio za ubingwa huku wakiiacha Azam FC ikijikongoja taratibu kusubiria vigogo hao mmoja atelezea ambapo jana timu hiyo iliambulia kichapo cha bao 1-0 mbele ya Pamba ya Mwanza.

## Kocha yaleta kocha mpya wa viungo

**Na Yassir Sudi**

UONGOZI wa klabu ya Yanga umemrejesha kwenye benchi la Ufundi aliyekuwa Kocha wa viungo wa timu hiyo Taibi Lagrouni (52) raia wa Morocco.

Tabi amerejea kwenye kikosi cha Yanga kuendelea kutumikia mkataba wake kama kocha wa viungo ambapo aliwekwa kando baada ya ujio wa aliyekua Kocha wa timu hiyo Sead Ramovic aliyekuja na kocha wake wa viungo Adnan Behlulovi.

Ofisa wa habari wa Yanga,alithibitisha ujio wa Kocha huyo akisema ni sehemu ya maboresho ya benchi la Ufundi kufanya mambo makubwa katika Ligi Kuu na michuano mingine ambayo timu hiyo inashiriki.



## Harry Kane anukia Arsenal

**NA ASHA SEKEFU**

Mshambulizi wa Uingereza Harry Kane,31,amekataa kuzungumza kuhusu ripoti kwamba anaweza kuhamia Arsenal mwaka ujao,kwa sababu ya kipengele cha kutolewa katika kandarasi yake ya Bayern Munich. (Mirror)

